

## Mpanda District Council

---

# REPORT ON THE EXERCISE OF ESTABLISHING A LOCAL AUTHORITY FOREST RESERVE FOR THE DISTRICT OF MPANDA

Date: 09–15/01/2013

### ***DISCLAIMER:***

Any unintended errors in the translation of the title and abstract of this report are inadvertent and the responsibility of the ABCG Secretariat and do not necessarily reflect views of TNC, its partners or any persons cited in the study.

### **1. INTRODUCTION**

The sensitization and advocacy exercise was held in two main phases. The first phase is an advocacy workshop at Ward level with stakeholders while the second was the public sessions and hearings for the villages bordering the area expected to be encompassed. The seminar was held on 01.09.2013 where the advocacy exercise in eight villages took place between tarehge 11-15/21/2013. The whole advocacy exercise went well and efficiently. In addition there were several of issues that were raised in the exercise.



## AFRICA BIODIVERSITY COLLABORATIVE GROUP

---



**USAID**  
FROM THE AMERICAN PEOPLE

**The Nature Conservancy**  
Protecting nature. Preserving life.<sup>TM</sup>

This report was made possible by the generous support of the American people through the United States Agency for International Development (USAID) under the terms of Cooperative Agreement No. RLA-A-00-07-00043-00. The contents are the responsibility of the Africa Biodiversity Collaborative Group (ABCG). Any opinions, findings, conclusions, or recommendations expressed in this publication are those of the authors and do not necessarily reflect the views of USAID or the United States Government. This publication was produced by **The Nature Conservancy** on behalf of ABCG.

**TAARIFA YA ZOEZI LA URGHIBISHI JUU YA KUTENGA MSITU WA  
HIFADHI WA HALMASHAURI YA WILAYA MPANDA  
TAREHE 09-15/01/2013**

**1. WAHUSIKA**

**1.1 Wataalamu**

Na	Jina la mshiriki	Cheo	Atokako
1	Josephine B Rupia	Kiongozi	Maliasili
2	Lucas Nyambala	Katibu	Misitu
3	Demitrius Kamtoini	Katibu Msaidizi	Leseni na Usuimamizi wa sheria za Misitu
4	Meckie Rojas	Mjumbe	Mipango Miji Ramani
5	Frank Kweka	Mjumbe	Mazingira
6	Japhet Kawimbe	Mjumbe	Sheria za Ardhi
7	Gadau	Mjumbe	Idara ya Maji
8	Devid	Dereva	Idara ya Maji

**1.2 Vijiji/Wakazi**

- 1) Lugonesi
- 2) Mwese
- 3) Lwega
- 4) Mpembe
- 5) Majalila
- 6) Vikonge
- 7) Bulamata
- 8) Isenga

**2. UTANGULIZI:**

Zoezi la Uraghishi limefanyika katika awamu mbili kuu. Awamu ya kwanza ni semina ya uraghiubishi katika ngazi ya Kata na tarafa wakati awamu ya pili ilikuwa vikao na mikutano ya hadhara kwa vijiji vinavyopakana na eneo linalitarajiwa kuhifadhiwa. Semina ilifanyika tarehe 09/01/2013 ambapo zoezi la uraghishi katika vijiji nane lilifanyika kati ya tarehge 11-15/21/2013. Zoezi zima la uraghishi lilikwenda vizuri na kwa ufanisi. Aidha yapo mambo kadhaa ya liyojitekeza katika zoezi zima la uraghishi.

**2. SEMINA YA URAGHIBISHI KATIKA NGAZI YA KATA NA TARAFA**

**2.1 Semina ya Uraghibishi**

Ilikujenga uelewa kwa viongozi wa Kata na Tarafa ambazo vijiji vyake vinapakana na eneo linalotarajiwa kuhifadhiwa semina maalum iliandaliwa na kufunguliwa na Mgeni rasmi Mhe

Wilbroad Mayala ambaye ni Mwenyekiti wa Halamshauri ya Wila ya Mpanda. PIA, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira alialikwa. Semina hii ni ya siku moja ambayo madhumuni yake yalikuwa kutoa uelewa kwa viongozi ngazi za Tarafa na Kata ili wajue ni nini Halmashauri yao inakusudia kufanya na wapi. Washiriki ni kama ifuatavyo;

- i. Tarafa: Ma katibu Tarafa wa Mwese na Kabungu
- ii. Kata Waheshimiwa Madiwani wa Kata za;
  - Katuma
  - Mwese
  - Mishamo na
  - Mpandandogo
- iii. Watendaji wa Kata;
  - Katuma
  - Mwese
  - Mishamo na
  - Mpandandogo
- iv. Wawakilishi wa wafadhili wa mhakato wa kuhifadhi msitu huria wa Tongwe Magharibi kuwa Msitu wa Hifadhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda yaani **JGI** na **TNC** walialikwa kama washiriki waangalizi (Observers).

Jumla ya mada tano ziliwasilishwa na wataalamu toka Halamshauri ya Wilaya ya Mpanda. Mada hizo ni;

- 1) Ufafanuzi wa kina juu ya lengo kuu la semina(Mtoa mada Nyambala, L.S.)
- 2) Jiografia ya msitu unaotarajiwa kuhifadhiwa (Mtoa mada Meckie Rojas)
- 3) Sheria zinazohusika katika zoezi zima la kuhifadhi msitu wa halmashauri ya wilaya ya mpanda;
  - Sheria ya wanyamapor(Mtoa mada Rupia JB.)
  - Sheria ya mazingira (Mtoa mada Kweka)
  - Sheria ya ardhi (Mtoa mada Japhet Kawimbe)
  - Sheria ya maji (Mtoa mada Enock Msengi)
  - Sheria ya misitu(Mtoa mada Demitrius Kamtoni)
- 4) Wajibu na nafasi ya washiriki wa semina katika kufanikisha lengo la halmashauri ya wilaya ya mpanda(Mtoa mada Patrick Mwakyusa)
- 5) Mpango kazi wa mchakato mzima (Mtoa mada Nyambala, L.S.)

## 2.2 Majumuisho

Kufuatia mwenendo wa maswali na majadilano ya mada zilizowasilishwa katika semina sekretariet iliandaa jedwali la majumuisho ya yaliyojitokezwa na maazimio yake kama jedwali lililoambatanishwa linavyoonyesha.

## 2.3 Tathimini ya Uraghribishi ngazi ya Tarafa na Kata

Tathimini ya semina ya uraghribishi ilifanyika tarehe 10/01/2013 kama ilivyopangwa ambapo wawezeshaji wakiwashirikisha wawakilishi wa wafadhili walijadili na kufasili baadhi ya maoni yaliyotolewa katika mijadala ya semina. Pamoja na hilo kikao hicho cha tathimini kilianisha mikakati ili kutekeleza maoni ya washiriki wa semina kwamba

mkakati madhubuti uandaliwe ili kujipanga jinsi msitu huo utakavyolindwa. Kwa ujumla wake yote yamejumuishwa kwenye jedwali la yatokanayo na semina.

### **3 ZIARA YA URAGHIBISHI NGAZI YA VIJII**

#### **3. 1 Malengo ya Ziara**

Ziara ya uraghibishi katika vijiji nane (8) iliyokuwa na dhumiuni la kujenga uelewa kwa wananchi wanaoishi kandokando ya eneo linalotarajiwa kuhifadhiwa. Malengo ya ziara hiyo ya uraghibishi iliyofanyika katika vijiji/makazi vya Lugonesi, Mwese, Lwega, Mpambe, Majalila, Vikonge, Bulamata na Isenga ni kama ifuatavyo:-

- 1) Kujulisha wananchi juu ya nia ya Halamshauri ya Wilaya ya Mpanda
- 2) Kujua mapokeo ya wananchi juu ya taarifa hii na kuongeza maarifa toka kwao
- 3) Kupata wawakilishi wao watakaoshiriki katika soroveya ya mipaka ya msitu
- 4) Kupata maoni yao jinsi tutakavyo fanya zoezi la soroveya ya mipaka na wazo zima la kuhifadhi msitu huo

#### **3. 2 Mwenendo wa Ziara**

##### **3.2.1 Kujulisha wananchi juu ya nia ya Halamshauri ya Wilaya ya Mpanda**

Wananchi wa vijiji vyote vinavyopakana na msitu unaotarajiwa kuhifadhiwa wameelewa maudhui ya ziara yetu ya kuwahabarisha nia ya Halmashauri ya Wila ya Mpanda kuhifadhi eneo la wazi (General Land) kuwa Msitu wa Hifadhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda.

##### **3.2.2 Kujua mapokeo ya wananchi juu ya taarifa hii na kuongeza maarifa toka kwao**

Nia ya Halmashauri ya wilaya ya Mpanda ilipokelewa vizuri katika vijiji vyote pamoja na uongozi wa Makazi ya Mishamo. Walifafanua kwamba kuna uvamizi katika maeneo hayo unaofanywa na wafugaji toka Shinyanga kwahiyio kuitenga msitu huo ilikuongeza udhibiti kutalinusuru pori hilo dhidi ya uharibifu unaoendelea.

##### **3.2.3 Kupata wawakilishi wao watakaoshiriki katika soroveya ya mipaka ya msitu**

Vijiji vyote vilikubali kutoa wawakilishi watakao shiriki pamoja na Kikosi Kazi cha Halmashuri ya Wilaya ya Mpanda cha kuendesha mchakato wa kulihifadhi eneo la wazi la Tongwe Magharibi kuwa Msitu wa Hifadhi utakaomilikiwa na Halmashauri ya Wila ya Mpanda. Kila Kijiji pamoja na Mkuu wa Makazi ya Wakimbizi ya Mishamo wamekubali kutoa wawakilishi wawiliwawili. Hii haihusishi Isenga na Bulamata kwakuwa vimo ndani ya Makazi.

### **3.2.4 Kupata maoni yao jinsi tutakavyo fanya zoezi la soroveya ya mipaka na wazo zima la kuhifadhi msitu huo**

Maeneo yote yalkiyopitiwa yalikuwa na neon mla kusema juu ya nia ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ya kuhifadhi eneo hilo. Maoni haya yamejumuishwa katika jedwali la yaliyojitokeza katika ziara. (Jedwali limeambatanishwa).

#### **Jedwali A; Yatokanayo na Ziara ya Uraghishi Vijijini**

KIJINI (MAKAZI)	HOJA	MAONI	MAAMUZI
Lugonesi	Zoezi la upimaji wa mipaka ya kijiji halijakamilika kwasababu msitu wa Ntakata umeachwa nje ya kijiji badala ya kuwekwa ndani ya kijiji.	Tunaruhusu mchakato uendelee lakini kabla ya kuanza upimaji wa eneo la msitu unaotarajiwa kuhifadhiwa, Mipaka ya kijiji cha Lugonesi ianze kupimwa kwanza.	Ratiba ya Soroveya itabadilishwa na kuanzia Lugonesi tarehe 18/01/2013
		Hivyo, mikutano mkuu ya Vijiji vya Lugonesi, Lwega na Mwese isubiri siku mtakayoanza zoezi la soroveya mipaka.	Mikutano hii itafanyika wakati zoezi la soroveya ya mipaka linaanza
Makazi ya Mishamo	Uongozi wa Makazi ya Wakimbizi ya Mishamo hautambui kuwepo kwa vijiji vya Isenga na Bulamata ndani ya Makazi bali kwamba ni vitongoji vya watanzania vilivyomo ndani ya Makazi ya Wakimbizi ya Mishamo kwasababu; ➤ Havina mipaka ndani ya Makazi ➤ Havina usajiri wa Kijiji	➤ Zoezi liendelee kwa kutambua kuwa ni vitongoji ndani ya Makazi ➤ Mkuu wa Makazi atatoa watu wawili kwaajili ya kusaidia kuitambua mipaka ya makazi	Wakati wa Soroveya mipaka tutawatumia wawakilishi tutakaopewa na mkuu wa Makazi ya Mishamo
Isenga	Hawatambui mipaka ya maeneo yao isipokuwa kwa msaada wa mkuu wa makazi	Uongozi wa Makazi utatoa watu wawili	“
Bulamamta	“	“	“

#### **4. HITIMISHO**

- ❖ Zoezi la Uraghibishi limekwenda vizuri kama lilivyopangwa na kwa mujibu wa ratiba
- ❖ Inashauriwa watumishi wanaoshiriki katika kutekeleza majukumu haya ya serikali wapewe motisha pale uwezekano unapokuwepo
- ❖ Watumishi washirikishwe katika hatua zote za kupanga na utekelezaji uzingatie mipango kama washiriki walivyoishiriki katika kupanga.

Nawasilisha

**K.n.y. KAIMU AFISA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MPANDA**